

## Maswali

1. Petro alifikiri eti anaweza kumsamehe mwenzake mara ngapi?
2. Yesu alimaanisha nini aliposema “Tusamehane sabini mara saba?”
3. Mbona Yesu alisema hadithi hii?
4. Mtumishi alidaiwa shilingi ngapi?
5. Angeweza kulipa hizo pesa?
6. Mbona mfalme alimuonea huruma?
7. Mtumishi mwingine alidaiwa shilingi ngapi?
8. Huyu mtumishi alifanyaje mtumishi mwenzake?
9. Mbona mfalme alimkasirikia huyo mtumishi?
10. Tunatakiwa tufanye nini ikiwa kuna mwenzetu tunayemdai pesa lakini hawezi kulipa?
11. Mbona tusamehe watu?

## Majibu

1. Petro alifikiri kwamba anatakiwa asamehe watu mara saba.
2. Yesu alimaanisha tunatakiwa tusamehe wenzetu kila wakati.
3. Yesu aliambia Petro hadithi kumsaidia aelewe kuhuzu msamaha.
4. Mtumishi alikuwa anadaiwa maelfu na maelfu ya pesa.
5. Mtumishi hangeweza kulipa hizo pesa kwa sababu zilikuwa ni nyingi kuliko mapato yake.
6. Mfalme alimhurumia kwa sababu alijua huu mkopo ulikuwa mkubwa na hangeweza kulipa, tena alimwona vile alikuwa ameogopa.
7. Mtumishi mwingine alidaiwa shilingi mia tatu.
8. Huyu mtumishi alitaka wamlipe hizo pesa. Alijaribu kumnyonga mwenzake, baadaye akamtupa gerezani.
9. Huyu mtumishi hakutaka kumsameha mwenzake hata kama mfalme alikuwa amemsamehe. Hii ilimkasirisha mfalme sana.
10. Ikiwa tunamdai mwenzetu pesa na hana tunapaswa kumsamehe. Soma Luka 6: 30-31.
11. Tunapaswa tuwasamehe wenzetu la sivyo, Mungu hawezi kutusameha sisi.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 2

# 34 Bwana anayesameha

**Marejeo** Mathayo 18: 21-25

## Kiini cha somo

Tujifunze kwamba Mungu hutusameha makosa na sisi pia tusamehe marafiki zetu

## Maneno maalum

1. Petro + Yesu + wangapi + saba + mara sabini + sameha kila wakati + changanyikiwa + hadithi + elewa
2. Mfalme + mtumishi + daiwa + pesa + malipo + mkopo
3. Maelfu + hangeweza + hurumia + kasirika + mtumishi + mke + watoto + uza + rudisha
4. Lia + pasa sauti + magoti + uoga + nivumilie + lipa kila kitu + mfalme alijua + hurumia + futa deni + simudai kitu + enda nyumbani + furahi sana
5. Mtumishi mwingine + dai pesa + nyonga + lipa + omba + nivumilie + lipa yote + kataa + gereza
6. Wafanyi kazi + hadithi ya huzuni + ghadhabu + mtumishi muovu + sameha + msamaha + mapenzi + kasirika + mtumishi asiyesameha + gereza
7. Mfalme + Mungu + sisi + watumishi + sameha + sisi kwa sisi


**34.1** Petro alimwendea Yesu na kumuuliza, “Ni mara ngapi nitamsameha ndugu yangu akinikosea? Mara saba?” Yesu alijibu na kumwambia, “La Petro, hiyo haitoshi! Unatakiwa umsamehe saba mara sabini.” Yesu alikuwa anaambia Petro pamoja na sisi kwamba tunatakiwa tusamehe wanaotukosea. Sio mara saba tu au mara sabini, lakini kila wakati. Hapa Petro alichanganyikiwa kwa hivyo Yesu akatumia hadithi ili aelewe.

**34.2** Kulikuwa na mfalme aliyekuwa na watumishi wengi na aliwadaa pesa ya mkopo. Aliamua kufanya uchunguzi. Akawa na mpango ili watumishi waje wamuone na wajipange vile watamlipa hiyo mikopo aliyowadaa.

**34.3** Mtumishi mmoja alikuja kwa mfalme. Alidaiwa maelfu na maelfu ya pesa. Hakujua afanye nini. Ilikuwa ni pesa nyingi sana. Hangeweza kupata hizi pesa zote pamoja. Alisema, “Nihurumie mfalme wangu! Sitaweza kulipa hizi pesa zote!” Mfalme alikasirika sana na akawaamrisha askari wamshike huyo mtumishi, mke wake na hata watoto wake wauzwe ili huo mkopo urudishwe.

**34.4** Huyo mtumishi alianza kulia na kupasa sauti. Kwa uoga alienda chini na kupiga magoti. “Tafathali mfalme wangu – Nivumilie nakuomba, usiniuze pamoja na familia yangu! Nitalipa kila kitu! O tafathali usiniuze.” Alilia. Mfalme alijua mtumishi hangeweza kumlipa hizo pesa kwa hivyo akamhurumia na kusema, “Najua hautalipa hizo pesa zote kwa hivyo naenda kufuta hilo deni.” Sikudai chochote! Enda nyumbani kwa familia yako.” Huyo mtu alifurahi sana. Hakuamini vile mfalme alikuwa mkarimu.

**34.5** Alipokuwa akiondoka kwa jumba la mfalme, aliona mmoja wa watumishi wenzake. Akamwambia huyo mtumishi mwenzake, “Una deni langu sivyo? Ninakudai shilingi mia tatu!” Alimshika kwa shingo na kuanza kumnyonga akisema, “Nilipe deni langu saa hii!” Mtumishi mwenzake alipiga magoti na kumuomba amvumilie. “Tafathali, nipe mda mchache na nitakulipa zote!” Alikataa kumhurumia na badala yake alimtupa gerezani mpaka alipe pesa zote.



**34.6** Wafanyi kazi wengine waliona haya yote na wakaenda kumwambia mfalme hadithi hii ya huzuni. Mfalme alighadhabika na akamuita yule mtumishi. Akamwambia, “Wewe mtumishi muovu. Nilikusamehe kwa sababu uliniomba. Ungesameha mtumishi mwenzako uliyemdaa pesa. Ungekuwa na upendo kwake kama vile nilikuwa nao kwako!” Mfalme alikasirikia sana yule mtumishi asiye na msamaha na akamueka gerezani mpaka alipe mkopo wote.

**34.7** Katika hadithi hii, mfalme ni kama Mungu. Sisi ni watumishi wake. Tusitarajie Mungu kutusameha kama sisi hatujasamehe wenzetu. Soma Mathayo 6: 14-15.